

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI MKWAWA
S.L.P 1363 IRINGA.**

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKWAWA

MWAKA 2021 KIDATO CHA KWANZA

Ninapenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika shule ya sekondari ya Mkwawa. Shule ya sekondari Mkwawa ni shule ya serikali inapatikana Mkoa wa Iringa, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa katika Kata ya Mkwawa Mtaa wa Ikonongo B.

Hii ni shule ya kutwa yenye wanafunzi mchanganyiko (wavulana na wasichana). Ina vidato vinne, kitato cha kwanza hadi cha nne.

Tarehe ya kuripoti shuleni **11/01/2021**

MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. SARE ZA SHULE

	WASICHANA	WAVULANA
1	Sketi ya malinda box pembeni ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu. Ziwe 2	Suruali yenye malinda na tanapu chini. Ziwe 2. (Upana wa chini wa suruali utoshe kupitisha chupa ya soda)
2	Mashati meupe mkono mifupi. Yawe 2	Mashati meupe mkono mifupi. Yawe 2
3	Sweta yenye "V" mbele, rangi ya jani la mgomba 1	Sweta yenye "V" mbele, rangi ya jani la mgomba
4	Traksuti nyekundu yenye miraba nyeupe pembeni	Traksuti nyekundu yenye miraba nyeupe pembeni
5	T-shirt ya kijivu 1	T-shirt ya kijivu 1
6	Soksi nyeupe jozi 3	Soksi nyeupe jozi 3
7	Raba nyeupe jozi 1	Raba nyeupe jozi 1
8	Viatu vyeusi vya kamba jozi 2	Viatu vyeusi vya kamba jozi 2

Mzazi hakikisha mwanao anajisitiri vizuri na anakuwa safi kila wakati.

2. VIFAA VYA KITAALUMA

- i. Daftari 'counter book quire 2' au zaidi. Ziwe 10
- ii. Daftari ndogo za msomi kwa ajili ya mazoezi. Ziwe 10
- iii. Mkebe 1
- iv. Rula 1
- v. English-English Dictionary 1
- vi. Bunda la karatasi nyeupe (Ream) 1

3. VIFAA VINGINE

- i. Picha 2 (passport size) awe amevaa shati jeupe
- ii. Nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa 1
- iii. Saa ya mkononi 1
- iv. Fagio kubwa ya chelewa yenye mti 1
- v. Jembe moja jipya lenye mpini kwa wasichana na Panga jipya kwa wavulana

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatavyo:

- a) Heshima kwa **viongozi, wazazi, wafanyakazi** wote, **wanafunzi** wote na **jamii** kwa ujumla ni jambo la **lazima**.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kuwahi katika shughuli za shule za nyingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- f) Kuvaa sare kamili ya shule wakati wote unapotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHIA UKAFUKUZWA SHULE.

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
- iii. Ulevi
- iv. Matumizi ya dawa za kulevya
- v. Kupiga au kupigana
- vi. Makosa ya jinai
- vii. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- viii. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
- ix. Kuoia au kuolewa
- x. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ya shule au nje ya shule
- xi. Kutoa mimba
- xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani
- xiii. Kukataa adhabu hali kwa makusudi
- xiv. Kumiliki simu
- xv. Matumizi ya lugha ya matusi

MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA

- a) ‘**Medical examination form**’ ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi/mlezi kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

ZINGATIA: Fomu hizi zijazwe kwa ukamilifu na kuletwa shuleni siku ya kuripoti shuleni.

.....
A.J. MAGOYO
MKUU WA SHULE